




duducoelho.com

# Mpango wa Taifa wa Vocha za Pembejeo za Kilimo

Sera ya kilimo ya Tanzania ya mwaka 2013 inaahidi kusaidia wakulima kuziendea pembejeo za Mapinduzi ya Kijani, na kuendeleza viwanda vya kuzalisha kemikali na mbolea za kilimo. **Mpango wa Taifa wa Vocha za Pembejeo za Kilimo (NAIVs)** ulizinduliwa mwaka 2008, lengo likiwa ni kuhamasisha matumizi ya mbolea sanisi (chumvi chumvi) kama njia ya kuongeza uzalishaji na uhakika wa chakula.

- NAIVs hutoa ruzuku ya asilimia 50 kwa mbegu zilizoboreshwa za mahindi/mpunga na mbolea, ili zipandwe kwenye 0.4hekta.
- Kamati za vocha za vijiji huchagua wanufaika na maafisa watendaji wa vijiji huzisambaza vocha hizo.
- Vocha zinaweza kununuliwa kwenye wauzaji binafsi wa pembejeo.
- Wauzaji wa pembejeo huzinunua vocha hizo kwenye makampuni ya pembejeo, na kisha kurudishiwa fedha zao na serikali.

Ili kufuzu kupata vifurushi wa NAIVs, wakulima ni lazima wawe wanashughulika na kilimo wakati wote, wawe wanalima 0.4hekta au chini yake, wawe wanapanda mahindi au mpunga, na wawe na uwezo wa kulipa asilimia 50 ya gharama za pembejeo.

african centre for biodiversity

www.acbio.org.za info@acbio.org.za Tel +27 (0)11 486 1156